



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**04/10/2021**

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb. Na FA.170/361/01"A"/162 cha tarehe 10/09/2021, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anawatangazia watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III-NAFASI TATU (3)**

**1.1 Sifa za mwombaji**

Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.2. Majukumu ya Mtendaji wa Kijiki Daraja la III**

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiki
- (ii) Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiki
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiki.
- (iv) Katibu wa Mikutano ya Kamati zote za Halmashuri ya Kijiki.
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiki.
- (viii) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Vijiki

**1.3 Ngazi ya Mshahara**

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS.B kwa mwezi

**1.4 Masharti ya ajira - (Ajira ya kudumu)**

